

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI

15 MEI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 15 MEI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

347. MHESHIMIWA OMARY MARCUS MSIGWA (MADABA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Walimu na Nyumba za Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari - Madaba.

348. MHESHIMIWA FAGASON ARON N KINGWA (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Ikunguigaze hadi Kiseke kwa Kiwango cha Lami.

349. MHESHIMIWA SILVERY LUBOJA SALVATORY (MISUNGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Watumishi wa Afya Misungwi kwa kuwa kuna upungufu wa asilimia sitini.

OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):

350. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Taasisi kama SIDO na VETA ili kuwajengea Vijana uwezo wa kujiajiri.

WIZARA YA NISHATI:

351. MHESHIMIWA ADONIS ALFRED BITEGEKO (MULEBA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, upi mpango wa kutatua tatizo la kukatika kwa umeme Wilaya ya Muleba linalosababishwa na miti kugusa nyaya za umeme.

352. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya Wachimbaji Wadogo ili kusaidia shughuli zao.

353. MHESHIMIWA ASHA SALUM MOTTO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina Vituo vingapi vya Gas nchini na vipo katika Mikoa gani.

WIZARA YA MAJI:

354. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASSINI CHIKAMBO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji katika Vijiji vya Mkalekawana, Msingili, Mkonda na Nambalapi katika Jimbo la Tunduru.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

355. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi na kuweka Samani katika Vituo vya Polisi Kata za Gwata, Soa na Kikongo – Kibaha Vijijini.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

356. MHESHIMIWA GRACE ELIAS MKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Kongani za Viwanda kwa Wilaya za Mkoa wa Singida.

357. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itatatia changamoto ya kukosekana kwa Viwanda vya kuchakata zao la Chai Tarafa ya Bungu - Korogwe Vijijini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

358. MHESHIMIWA DKT. REGINA CHRISTOPHER MALIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya tathmini na kukiweka Kisiwa cha Ukerewe chenye Visiwa 38 ndani yake kwenye Vivutio vya Kiutalii nchini.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

359. MHESHIMIWA TINNAR ANDREW CHENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia :-

Je, Serikali inachukua hatua gani kubaini chanzo cha tabia ya Wanafunzi kuandika lugha zisizo na staha kwenye karatasi za mitihani.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

DODOMA
15 MEI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE